

# جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية الجاليات بالزلفي

## مشروع تعلم الإسلام - أصول العقيدة - سواحيلي

Samo la 1

الدرس الأول

### TAUHEED NA AINA ZAKE.

Maana ya Tauheed. Tauheed ni kumpwekesha Allah (sw) kwa yale ambayo ni khasa kwake yeye, ambayo ni wajibu katika aina za ibada, na hiyo tauheed ni katika jambo kubwa aliloliamrisha Allah (sw), Allah anasema katika quran:

قال الله تعالى: ﴿ قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴾ [الإخلاص: ۱]

("Sema ye ye Allah ni mmoja tu") ( ikhlas : 1).

وقال سبحانه: ﴿ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّةِ وَالْإِنْسَانَ إِلَّا لِيَعْبُدُونَ ﴾ [الذاريات: ۵۶]

Allah (sw) anasema: ("Sikuwaumba majini na binadamu isipokuwa ni kwa lengo la kuniabudu") (Adhariyat : 56).

وقال سبحانه: ﴿ وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا شَرِكُوا بِهِ شَيْئًا ﴾ [النساء: ۳۶]

akaema tena Allah (sw) : ("Mwabuduni Allah wala msimshirikishe na chochote ") (Alnnisah: 36).

Tauheed imegawanyika vigawanyo vitatu (3) ;

1. Tauheed Rubuubiyah ( Ulezi wa Allah )
2. Tauheed Uluhiyyah ( Uungu wa Allah)
3. Tauheed Asmai wa swifat ( majina ya Allah na sifa zake)

### 1 : TAUHEED ALRUBUBIYYAH.

Maana yake ni kumpwekesha Allah (sw) katika kuumba, kuiendesha hii dunia, na kwamba ye ye Allah ndiye mwenye kutoa riziki, mwenye kuhuyisha na kufisha, ndiye mwenye kumiliki mbingu saba na ardhi saba.

قال تعالى: ﴿ هَلْ مِنْ خَالِقٍ غَيْرُ اللَّهِ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَإِنَّى تُؤْفَكُونَ ﴾ [فاطر: ۲]

Allah (sw) anasema : ("..... Hakuna muumba wenu zaidi ya mwenyezi mungu anaye awaruzuku nyinyi kwa mvua kutoka mbinguni, hapana mola isipokuwa ye ye peke yake, basi vipi nyinyi mtaepushwa na kumpwekesha?") ( Fatir : 3 ).

وقال: ﴿ تَبَارَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴾ [الملك: ۱]

Allah anasema: ("Ametakasika yule ambaye mikonomi mwake upo ufalme wa duniani na Akhera, na ye ye kwa kila jambo nimuweza") (Al-Mulk:1).

Na ufalme wake Allah (sw) ni ufalme uliokusanya kila kitu vilivymo hapa duniani na kuviswarifu atakavyo.

Ama kumpwekesha Allah (sw) katika kuendesha mambo yote Duniani ni kumpwekesha katika kuumba kwake.

قال سبحانه: ﴿ أَلَا لَمْ يَخْلُقْ وَالْأَمْرُ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴾ [الأعراف: ۵۴]

Anasema Allah (sw) (..... " Uumbaji wote ni wake na ni yake ye ye amri, ametukuka mwenyezi mungu bwana wa viumbi wote") (Al-a'raf:56).

Kuendesha mambo kuliko kamiliya na kunakokusanya mambo ya viumbi wote.

Na hakuna waliokataa kuamini Tauheed hii isipokuwa kundi mionganini mwa wanaadamu, waliikataa hii tauheed wazi wazi, lakini nafsi zao zilikubali na kuikiri.

قال تعالى: ﴿ وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنُتْهَا أَنْفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا ﴾ [التحليل: ۱۴]

Allah (sw) anasema : (" Na walikanusha Firauna na watu wake, na hali ya kuwa wana yakini ndani ya nyoyo zao, kwa kuifanyia uadui haki na kuwa na kiburi cha kutoikubali") ( An-naml : 14).

Kupwekesha peke yake hakumfai mtu, kama vile ambavyo hawakunufaika washirikina kwa kukiri kwao hii Tauheed Rububiyyah.

قال الله عنهم: ﴿ وَلَئِنْ سَأَلْتُهُمْ مَنْ حَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ فَإِنِّي يُؤْفَكُونَ ﴾ [العنكبوت: ۶۱]

Allah (sw) anasema : ( " Ukiwaliza ewe Mtume hao washirikina, ni nani aliyeumba mbingu na ardhi kwa mpango huu mzuri na akalidhalilisha jua na mwezi, watasema ni alieviumba hivyo ni mwenyezi mungu peke yake, basi vipi wao watapotoshwa waache kumuamini mwenyezi mungu.") ( Al-ankabut:61).